

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Simu: +255 26 2322761-5
Fax No. +255 26 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz



BUNGE LA TANZANIA

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S. L. P. 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MKUTANO WA TANO WA BUNGE LA KUMI NA TATU (13)

Mkutano wa Tano (5) wa Bunge la Kumi na Tatu (13) unatarajiwa kuanza Siku ya Jumanne tarehe 27 Oktoba, 2026 Jijini Dodoma na kuahirishwa Siku ya Ijumaa tarehe 6 Novemba, 2026. Shughuli zitakazofanyika katika Mkutano huu ni pamoja na:-

a) Maswali

Kama ilivyo ada katika kila Mkutano wa Bunge kunakuwa na kipindi cha Maswali Bungeni kila siku ambapo jumla ya maswali 160 yataulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Mawaziri. Aidha, kutakuwa na kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu siku ya Alhamisi ambapo takriban maswali kumi na sita (16) yataulizwa na Waheshimiwa Wabunge.

b) Maazimio ya Bunge

Katika Mkutano wa Tano (5) wa Bunge, jumla ya maazimio matatu (3) yatawasilishwa na kujadiliwa na Bunge kwa ajili ya kupitishwa. Maazimio hayo ni:-

- (i) Azimio la Bunge la Kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Kuridhia na Kuwezesha kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyika Jijini Arusha kuanzia Tarehe 5 – 9 Oktoba 2026.
- (ii) Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kimataifa wa Sukari wa Mwaka 1992 (International Sugar Agreement of 1992).
- (iii) Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Tanzania Kujiunga na Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Usalama wa Angamtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2014 (Mkataba wa Malabo)



c) Kamati ya Mipango

Katika Mkutano huu, Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango kwa ajili ya kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

d) Taarifa za Kamati

Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) zitawasilisha taarifa za Kamati hizo kuhusu Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji wa Umma (PIC) itawasilisha taarifa ya Kamati hiyo kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Ratiba ya shughuli zote zitakazofanyika katika Mkutano wa Tano (5) wa Bunge inapatikana katika tovuti ya Bunge ambayo ni **www.bunge.go.tz**

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
DODOMA.

26 Oktoba, 2026.

